

# MAIR

Ripoti ya Mwaka ya Utekelezaji  
MKUKUTA - 2006/2007



**Nguzo ya Pili:**  
**Uboreshaji wa Maisha na**  
**Ustawi wa Jamii**

**Nguzo ya pili** ya MKUKUTA hushughulikia shughuli zinazokuza “Uboreshaji wa Maisha na Ustawi wa Jamii” . Matokeo ya jumla yatakuwa (a) Kuboreka kwa maisha na ustawi wa jamii msisitizo wa kipekee ukiwa kwa watu maskini zaidi pamoja na wale waliokatika mazingira hatarishi. (b) kupungua kwa tofauti ya kimatokeo (mfano; elimu, na afya) kwa kuzingatia maeneo ya kijiografia, kipato, umri, jinsia, na makundi mengine

## **Malengo:**

- Kuhakikisha upatikanaji sawa wa elimu bora ya msingi na sekondari kwa wavulana na wasichana, elimu ya kufuta ujinga miongoni mwa wanaume na wanawake, na upanuzi wa elimu ya juu, elimu ya ufundi na ufundi stadi.
- Kuboresha maisha, afya na ustawi wa watoto wote na wanawake hususan makundi yaliyo katika mazingira hatarishi.
- Kuongeza upatikanaji wa maji safi, salama naya gharama nafuu, usafi, malazi bora, na mazingira salama na endelevu; na hivyo kupunguza uathirikaji utokanao na hatari za mazingira.
- Kuhakikisha kunakuwapo hifadhi ya uhakika ya kijamii na utoaji wa mahitaji na huduma za msingi kwa wahitaji na walio katika mazingira hatarishi.
- Kuhakikisha kunakuwepo mifumo madhubuti inayoruhusu watu wote kupata huduma za umma zilizo bora na rahisi.

## **Changamoto kuu**

Ili kufikia malengo, inatupasa kuzishughulikia changamoto zifuatazo:

- Ubora wa Elimu
- Usawa wa kijinsia katika elimu
- Huduma bora za afya
- Huduma bora za maji na usafi wa mazingira
- Kushughulikia mahitaji ya watu walio katika mazingira hatarishi
- Kuhakikisha katika sekta za huduma kunakuwa na wafanyakazi waliosomea fani hizo

## **Mambo Tuliyojifunza**

Mtazamo wa MKUKUTA wa kuzingatia matokeo unawezesha kubainisha mwelekeo mtambuka wa juhudi nyingi za kimaendeleo.

### ***Elimu***

Kuongeza asilimia ya walimu wenye sifa zinazotakiwa ni sharti muhimu la kukuza ubora wa elimu. Hata hivyo sharti hili halijitoshelezi peke yake.

### ***Afya***

Kumekuwepo na mafanikio katika kupunguza utapiamlo, vifo vya watoto wachanga na walio chini ya umri wa miaka mitano, na kudumaa. Hili limechangiwa kwa kiasi kikubwa na utoaji wa chanjo, ikihusiana na uboreshaji wa lishe.

### ***Maji na Nishati***

Upatikanaji duni wa huduma za jamii kama vile maji na vyanzo mbadala vya nishati kukwamisha juhudi za kupata elimu katika ngazi ya kaya/familia, hususan kwa wanawake. Muda mwingi unaotumika kaatika kuchota maji na kutafuta nishati kama vile kuni ungeweza kutumika kwa shughuli nyingine.

### ***Wafanyakazi Wenye Sifa***

Maeneo mengi ya vijijini hayana huduma nzuri kwa watumishi, ikiwa ni pamoja na nyumba za kuishi. Hali hii inawakatisha tama wafanyakazi katika sekta ya huduma za jamii wenye sifa kufanya kazi katika maeneo hayo.

### ***Ushiriki wa Jamii***

Malengo mengi ya nguzo ya pili hayatafikiwa kutokana na ushiriki mdogo wa wananchi. Mchango wa ushiriki wao katika kupanga, mchango wa hali na mali katika miradi ya maendeleo ni muhimu sana hivyo taratibu zinapaswa kuwekwa ili kuongeza ushiriki wao.

## Hatua za kuchukua

Hatua zinazopaswa kuchukuliwa zinahusisha kukabiliana na changamoto zilizotajwa hapo juu. Maeneo muhimu yafuatayo yanahitaji hatua za makusudi:

- Changamoto zinabainisha hitaji la kuongeza ushiriki wa wadau ili kuharakisha uchukuaji wa hatua zitakazosaidia kufikiwa kwa malengo ya MKUKUTA
- Kuna umuhimu wa kuongeza upanuzi na ubora wa elimu kwa kuongeza idadi ya walimu wenye sifa, na kuongeza vifaa vya kujifunza na kufundishia mashuleni. Pia kuna umuhimu wa kuondoa tofauti za kijinsia katika ngazi zote za elimu.
- Mafunzo kwa watumishi wa umma hayana budi kuendelea ili kuimarisha usimamizi wa raslimali za umma. Kutakuwa na mafunzo kwa njia ya masafa kwa watumishi wa sekta ya huduma za jamii, hususan wale walioko vijijini.
- Juhudi za maksudi zinahitajika miongoni mwa wadau wa afya ili kugeuza maendeleo hasi katika vifo vya kinamama wazazi na katika suala zima la VVU na UKIMWI.
- Hapana budi kuandaliwa miongozo na mifumo ya kuyafanya masuala ya watoto yatima na wale walio katika mazingira hatarishi kuwa mtambuka. Miongozo hiyo inapaswa kuhusisha kuwajengea uwezo maofisa husika katika kushughulikia masuala ya watu wenye ulemavu na wazee. Kuna umuhimu mkubwa wa kuboresha mipango ya hifadhi ya kijamii kwa makundi yaliyo katika mazingira hatarishi. Juhudi za kuongeza upanuzi na uboreshaji wa huduma za jamii kupitia ubia wa sekta ya umma na ya binafsi hazina budi kuendelezwa.
- Kampeni ya mazingira inapaswa kupanuliwa ili kuongeza ufahamu wa wadau juu ya hifadhi ya mazingira.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na:**

Wizara ya Fedha na Uchumi,  
S..L.P. 9111, Dar Es Salaam

Simu: +255 2111174, Fax: 21103226

Barua Pepe: [mkukuta@gmail.com](mailto:mkukuta@gmail.com); Tovuti: [www.povertymonitoring.go.tz](http://www.povertymonitoring.go.tz)